Wananchi wanasemaje kuhusu uhuru wa vyombo vya habari nchini Tanzania?

Takwimu zilizotumika zinatoka katika vyanzo vikuu viwili; *Sauti za Wananchi,* utafiti wenye uwakilishi wa kitaifa unaotumia simu za mikononi, huwakilisha Tanzania bara pekee, na *Afrobarometer,* utafiti mkubwa barani Afrika unaokusanya maoni ya wananchi kuhusu masuala ya kiuchumi na kisiasa. *Afrobarometer* hufanyika kila baada ya miaka 2-3 una uwakilishi wa Tanzania Bara na Tanzania Visiwani.

Jambo la 1: Wananchi wengi wanaunga mkono demokrasia

Uchaguzi wa kidemokrasia umekuwa ukiungwa mkono kwa kiwango kikubwa. *Afrobarometer* inaonyesha kuwa 74% - 90% ya Watanzania wanasema demokrasia ni mfumo wa serikali wanaoukubali kuliko mifumo mingine. Utafiti wa *Sauti za Wananchi* unaonyesha kiwango hicho hicho cha wananchi kuunga mkono demokrasia.



Chanzo: Sauti za Wananchi, 2016



Chanzo: Afrobarometer, 1999 - 2014



Chanzo: Afrobarometer, 2002 - 2014

Jambo la 2. Wananchi kumi na tisa kati ya ishirini wanasema uhuru wa kujieleza

Uungaji mkono uhuru wa kuzungumza ni mkubwa. Idadi kubwa ya wananchi (95%) wanasema wananchi waruhusiwe kuikosoa serikali pale wanapoona imekosea.



Chanzo: Sauti za Wananchi, 2016

Jambo la 3: Wananchi wanasema vyombo vya habari viwe huru kufanya kazi bila kuingiliwa na serikali

Asilimia 53 ya wananchi wanasema kuwa kuvipa uhuru vyombo vya habari kufanya kazi bila kuingiliwa ni muhimu. Hii inatokana na serikali kuwa na mamlaka ya kufungia magazeti pale yanapochapisha taarifa zinazoikera serikali (yenyewe). Uungaji mkono wa uhuru wa vyombo vya habari umekuwa ukitofautiana kidogo katika kipindi cha miaka kumi iliyopita. Hata hivyo, asilimia kubwa ya wananchi wameonyesha kuunga mkono uhuru wa vyombo vya habari toka mwaka 2008.



Chanzo: Afrobarometer, 2005 - 2014

Jambo la 4: Wananchi wanaona faida za kuwa na vyombo vya habari makini

Idadi kubwa ya wananchi wanasema kuna faida kubwa kwa nchi kama maovu yanayofanywa na serikali yatatangazwa . Utafiti wa hivi karibuni wa *Afrobarometer* (2013/14) umegundua kuwa theluthi mbili ya wananchi (65%) wanasema ni muhimu masuala hayo kutangazwa.



Chanzo: Afrobarometer, 2008 - 2014

Jambo la 5: Wananchi watatu kati ya wanne wanasema vyombo vya habari vinaweza kutumika kuiwajibisha serikali; ni mwananchi mmoja tu kati ya wanne anayesema vyombo vya habari hutumia vibaya uhuru wake.

Uungaji mkono wa uhuru wa vyombo vya habari unapigiwa chapua na maoni ya wananchi kuhusu utendaji wa vyombo vya habari. Wananchi watatu kati ya wanne wanasema vyombo vya habari vinafanya vizuri sana au kwa kiasi fulani katika kufichua maovu ya serikali na rushwa.

Vilevile, wananchi wawili kati ya watatu wanasema kuwa vyombo vya habari havijawahi au mara chache sana hutumia vibaya uhuru wake kutangaza mambo ambayo wanafahamu siyo ya kweli.



Chanzo: Afrobarometer, 2011 - 2014

Jambo la 6. Idadi kubwa ya wananchi wanapinga uamuzi wa kusitisha matangazo ya moja kwa moja kutoka bungeni.

Wananchi wengi wanatambua umuhimu na uhuru wa kupata taarifa. Wananchi nane kati ya kumi (79%) wanapinga uamuzi wa serikali wa kusitisha matangazo ya bunge ya moja kwa moja kupitia runinga na radio. Vilevile, wananchi tisa kati ya kumi (92%) wanasema ni muhimu matangazo ya bunge yakarushwa moja kwa moja kupita runinga na radio. Huku, wananchi tisa kati ya kumi (88%) wakisema gharama isitumike kama sababu ya kusitisha matangazo hayo.



Chanzo: Sauti za Wananchi, 2016

Jambo 7: Robo tatu ya wananchi wanaona upatikanaji wa habari kama njia ya kupambana na rushwa na uongozi mbaya

Wananchi 8 kati ya 10 (80%) wanasema uhuru wa kupata taarifa ungesaidia kupunguza vitendo vya rushwa. Idadi kama hiyo (77%) wanaunga mkono haki ya wananchi kupata taarifa za serikali. Vyombo vya habari ni njia mojawapo ambayo wananchi wanaweza kutumia kupata taarifa hizo.



Chanzo: Sauti za Wananchi, 2016